

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

**BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA
NISHATI NA MAJI (EWURA CCC)**



**MAONI YA BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA CCC) JUU YA OMBI LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA
TANGA LA KUTAKA KUPANDISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI KWA KIPINDI CHA
MIAKA MITANO KUANZIA 2026/27-2030/31**

1. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA Consumer Consultative Council – EWURA CCC) linapenda kuwasilisha maoni yake kuhusu ombi la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) la kuidhinishiwa mapitio ya bei za huduma za maji kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2026/27 hadi 2030/31.

Maoni haya yametokana na mapitio ya nyaraka mbalimbali zilizowasilishwa na Tanga UWASA, zikiwemo:

- i. Maombi ya Mapitio ya Bei (Tariff Application);
 - ii. Mpango wa Biashara (Business Plan);
 - iii. Muhtasari wa Kikao cha Wadau (Stakeholder Consultation Minutes);
 - iv. Azimio la Bodi;
 - v. Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2024/25;
 - vi. Taarifa ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG Report);
 - vii. Barua ya Wizara ya Maji ya kutokuwa na pingamizi (No Objection Letter); na
 - viii. Kanuni za EWURA.
2. Baraza limepitia Ombi la Mapitio ya Bei la Tanga UWASA na kubaini kuwa Mamlaka inapendekeza kuongeza wastani wa bei ya huduma za maji kutoka Shilingi 1,931 kwa mita ya ujazo hadi Shilingi 3,101 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27, sawa na

ongezeko la takribani asilimia 61. Wastani huo unapendekezwa kuongezeka hadi Shilingi 3,273 mwaka 2027/28, Shilingi 3,350 mwaka 2028/29, Shilingi 3,448 mwaka 2029/30 na Shilingi 3,579 mwaka 2030/31 (Tariff Application, Form 1A, uk. 8–9).

Hata hivyo, Baraza limebaini kuwa bei ya Shilingi 1,931 ni wastani uliorekebishwa wa eneo la huduma, wakati bei za sasa zinatofautiana kati ya maeneo yanayohudumiwa na Tanga UWASA. Form 1A inaonesha, wastani wa bei ya sasa ni Shilingi 1,983 kwa mita ya ujazo Tanga City, Shilingi 1,243 Muheza na Shilingi 1,211 Pangani. Hivyo, athari ya bei inayopendekezwa haiwezi kutathminiwa kikamilifu kwa kutumia ongezeko la wastani la asilimia 61 pekee (Tariff Application, Form 1A, uk. 8–9).

Baraza limebaini pia kuwa Tanga UWASA inapendekeza kubadilisha muundo wa sasa wa bei kwa kuondoa madaraja ya matumizi na kuweka kiwango kimoja cha bei kwa kila kundi la watumiaji katika eneo lote la huduma. Kwa mfano, watumiaji wa majumbani Tanga City kwa sasa wanalipa kati ya Shilingi 1,710 na 2,285 kwa mita ya ujazo kulingana na matumizi, wakati Muheza wanalipa Shilingi 1,150 au 1,250 kwa mita ya ujazo kulingana na matumizi. Bei inayopendekezwa kwa watumiaji wa majumbani katika eneo lote la huduma ni Shilingi 3,000 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27 (Tariff Application, Form 1A, uk. 8–9).

Kwa mtazamo wa Baraza, mabadiliko hayo yana athari mbili zinazopaswa kutathminiwa kwa pamoja. Kwanza, ni ongezeko la viwango vya bei; na pili, ni kuondolewa kwa madaraja ya matumizi na kuunganishwa kwa viwango tofauti vya bei vilivyopo katika maeneo mbalimbali kuwa muundo mmoja wa bei. Kwa sababu hiyo, athari halisi kwa mtumiaji zinaweza kutofautiana kulingana na eneo, kundi la mtumiaji na kiasi cha maji anachotumia.

Hata hivyo, Baraza halikuona katika nyaraka zilizowasilishwa uchambuzi unaoonesha kwa kina athari za mabadiliko hayo katika bili za watumiaji. Hususan, hakuna uchambuzi unaotenganisha Tanga City, Muheza na Pangani na kuonesha kiasi ambacho watumiaji katika viwango mbalimbali vya matumizi wanalipa sasa na kiasi watakacholipa baada ya bei mpya kuanza kutumika.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuitaka Tanga UWASA kuwasilisha uchambuzi wa athari za bei katika bili za watumiaji, ukitenganisha Tanga City, Muheza na Pangani, makundi ya watumiaji na viwango mbalimbali vya matumizi;
 - ii. Kujiridhisha kuhusu msingi uliotumika kupata wastani uliorekebishwa wa Shilingi 1,931 kwa mita ya ujazo, na kuhakikisha kuwa ongezeko la asilimia 61 halitumiki kama kipimo pekee cha athari za bei kwa watumiaji;
 - iii. Kutathmini athari za kuondolewa kwa madaraja ya matumizi, hususan kwa kaya zenye matumizi madogo ya maji; na
 - iv. Kujiridhisha kuwa kuunganishwa kwa viwango tofauti vya bei katika muundo mmoja hakutasababisha athari zisizo na uwiano kwa baadhi ya watumiaji, hususan kaya zenye matumizi madogo na zenye kipato cha chini.
3. Nyaraka za Tanga UWASA, zinaeleza moja ya misingi iliyozingatiwa katika kuandaa mapendekezo ya bei ni kuhakikisha kunakuwa na uwiano kati ya uwezo wa watumiaji kumudu gharama za huduma, urejeshaji wa gharama za uendeshaji na uendelevu wa kifedha wa Mamlaka (Business Plan, Executive Summary, uk. ix).

Hata hivyo, wakati wa mapitio ya nyaraka zilizowasilishwa, Baraza halikuona uchambuzi wa kina unaoonesha uwezo wa kaya na makundi mbalimbali ya watumiaji kumudu ongezeko la bei linalopendekezwa na Mamlaka. Aidha, Baraza halikuona taarifa zinazoonesha mapato ya kaya zinazohudumiwa na Tanga UWASA, uwiano kati ya bili za maji na mapato ya kaya, wala uchambuzi unaoonesha athari za bei mpya kwa kaya zenye kipato cha chini.

Suala hili ni muhimu zaidi kwa Muheza na Pangani, ambako, kama ilivyoelezwa katika Hoja Na. 2, wastani wa bei za sasa ni wa chini zaidi kuliko wastani wa bei unaopendekezwa kwa eneo lote la huduma. Kwa kulinganisha wastani wa sasa na wastani unaopendekezwa wa Shilingi 3,101 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27, ongezeko linafikia takribani asilimia 149 kwa Muheza na asilimia 156 kwa Pangani. Hivyo, tathmini ya uwezo wa kumudu gharama inapaswa kuonesha iwapo watumiaji

wa maeneo hayo wataweza kumudu mabadiliko hayo (Tariff Application, Form 1A, uk. 8–9)

Baraza pia halikuona katika nyaraka zilizowasilishwa matokeo ya utafiti kuhusu utayari wa watumiaji kulipia huduma, ambao ungewezesha kutathmini kiwango ambacho watumiaji wako tayari kulipia kwa kuzingatia huduma wanazopokea na maboresho yanayotarajiwa kutokana na bei mpya.

Aidha, Mpango wa Biashara unaonesha kuwa bado kuna maeneo yasiyohudumiwa kikamilifu, yakiwemo baadhi ya maeneo ya Muheza na Pangani, na Tanga UWASA inalenga kupanua huduma katika maeneo hayo (Business Plan, Appendix C, uk. 372–373). Mamlaka pia imepanga kuunganisha wateja wapya 2,350 kwa mwaka, wakiwemo 150 Mji wa Muheza na 100 Mji wa Pangani (Business Plan, uk. 60; Implementation Plan, uk. 97).

Baraza linaona kuwa, ongezeko kubwa la gharama za huduma katika maeneo ambayo Mamlaka pia inalenga kuongeza idadi ya wananchi wanaounganishiwa huduma linahitaji kutathminiwa kwa makini. Gharama ambazo watumiaji hawawezi kumudu zinaweza kuwa kikwazo kwa wananchi kuunganishiwa huduma au kuendelea kutumia huduma baada ya kuunganishwa.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuitaka Tanga UWASA kuwasilisha uchambuzi wa uwezo wa watumiaji kumudu gharama za huduma, ukitenganisha athari kwa Tanga City, Muheza na Pangani, na kwa makundi mbalimbali ya watumiaji;
- ii. Kuhakikisha kuwa uchambuzi huo unaonesha uhusiano kati ya bili zinazotarajiwa na uwezo wa kaya kumudu gharama hizo, hususan kwa kaya zenye kipato cha chini;
- iii. Kujiridhisha mahsusi kuhusu uwezo wa watumiaji wa Muheza na Pangani kumudu bei inayopendekezwa, kutokana na ukubwa wa ongezeko linaloashiriwa na tofauti kati ya wastani wa bei za sasa na wastani unaopendekezwa;

- iv. Kuitaka Tanga UWASA kuwasilisha matokeo ya utafiti kuhusu utayari wa watumiaji kulipia huduma, iwapo utafiti huo umefanyika, au ushahidi mwingine unaonesha namna uwezo na maoni ya watumiaji yalivyozingatiwa katika kuandaa mapendekezo ya bei; na
 - v. Kuhakikisha kuwa bei zitakazoidhinishwa hazitakuwa kikwazo kwa lengo la kuongeza wananchi wanaounganishiwa huduma, hususan katika maeneo ya Muheza na Pangani ambayo Mpango wa Biashara umeyatambua kuwa yanahitaji upanuzi wa huduma.
4. Ombi la Mapitio ya Bei pamoja na Mpango Biashara wa Tanga UWASA vimebainisha moja ya sababu zinazotolewa kuhalalisha ongezeko la bei ni wajibu wa kifedha unaotokana na Hati Fungani ya Kijani (Green Bond), iliyotumika kugharamia miradi ya maji na usafi wa mazingira.

Taarifa zilizomo kwenye Wasilisho la Maombi ya Mapitio (Tariff Review Application) ya Tanga UWASA zinaonesha kuwa, Mamlaka hii inatarajia kulipa **riba ya Hati Fungani ya Shilingi 7,171,200,000** kwa mwaka, pamoja na **kuchangia Mfuko wa Akiba wa Kulipa Hati Fungani kiasi cha Shilingi 7,588,571,428** kwa mwaka kuanzia mwaka 2026/27. Hivyo, jumla ya takribani **Shilingi bilioni 14.760** kwa mwaka inahitajika kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo ya kifedha (Tariff Application, uk. 4).

Baraza linatambua kuwa baadhi ya miradi inayofadhiliwa kupitia Hati Fungani inalenga kuboresha huduma katika maeneo mbalimbali ya Tanga UWASA. Kwa mfano, Mpango Biashara unaonesha mradi wa kupanua kilomita 60 za mtandao wa maji, ambapo kilomita 30 ni Tanga City, kilomita 15 Muheza na kilomita 15 Pangani. Aidha, mradi wa kubadilisha kilomita 110 za mabomba ya zamani na yaliyochakaa unahusisha Tanga City, Muheza na Pangani pamoja na ununuzi wa mita 10,000 za malipo kabla (Business Plan, uk. 369–370).

Hata hivyo, taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa miradi hiyo ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa mradi wa kilomita 60, kilomita 18 zilikuwa zimetandazwa katika Tanga City, Muheza na Pangani, wakati katika mradi wa

kubadilisha kilomita 110 za mabomba, kilomita 8.5 zilizokuwa zimefanyiwa ukarabati zilikuwa Tanga City (Business Plan, uk. 369–370).

Baraza linaona kuwa, hali hii ni muhimu katika tathmini ya bei, hususan kwa Muheza na Pangani, ambako kama ilivyooneshwa katika Hoja Na. 2, mabadiliko kutoka wastani wa bei za sasa kwenda wastani unaopendekezwa yanaashiria ongezeko kubwa zaidi. Hivyo, pamoja na kuhakiki wajibu wa kifedha wa Hati Fungani, ni muhimu EWURA ijiridhishe kuhusu hatua ya utekelezaji, mgawanyo wa uwekezaji na manufaa yanayotarajiwa kwa watumiaji katika kila eneo.

Aidha, Baraza limebaini kuwa nyaraka zilizowasilishwa hazijaonesha kwa uwazi mgawanyo wa gharama zinazotokana na Hati Fungani kati ya riba, Mfuko wa Akiba wa Kulipa Hati Fungani, uchakavu wa mali, gharama za uendesaji na gharama nyingine za miradi. Bila uchambuzi huo, ni vigumu kujiridhisha iwapo gharama zinazohusiana na Hati Fungani zinarejeshwa mara moja tu kupitia bei.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa gharama zote zinazotokana na Hati Fungani zimeainishwa kwa uwazi na hazirejeshwi kwa watumiaji zaidi ya mara moja kupitia riba, Mfuko wa Akiba, uchakavu wa mali au vipengele vingine vya bei;
- ii. Kuhakiki hali ya utekelezaji wa kila mradi unaofadhiliwa kupitia Hati Fungani na mgawanyo wa uwekezaji na manufaa yake katika Tanga City, Muheza na Pangani;
- iii. Kujiridhisha kuwa gharama za uwekezaji zinazorejeshwa kupitia bei zinaendana na hatua ya utekelezaji wa miradi na manufaa yanayopatikana kwa watumiaji; na
- iv. Kuhakikisha kuwa, hususan kwa Muheza na Pangani, ongezeko la bei linaambatana na utekelezaji wa maboresho ya miundombinu na huduma yaliyopangwa katika maeneo hayo.

5. Kwenye makadirio ya gharama za uendeshaji yaliyowasilishwa na Tanga UWASA pamoja na maelezo ya sababu za kuomba mapitio ya bei, Mamlaka imeeleza kuwa gharama za uendeshaji zimeongezeka kwa kiasi kikubwa tangu bei ya sasa ilipoanza kutumika mwaka 2020, hususan kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa na huduma muhimu zinazotumika katika uzalishaji na usambazaji wa maji.

Aidha Wasilisho la Mapitio ya Beo linaonesha kuwa wastani wa bei za pembejeo muhimu umeongezeka kwa takribani asilimia 102. Gharama za baadhi ya kemikali za kutibu maji zimeongezeka kwa takribani asilimia 96, vifaa vya maabara kwa asilimia 102, mabomba kwa asilimia 138, vifaa vya mabomba kwa asilimia 99, huku baadhi ya vipuri vya mitambo vikionesha ongezeko linalozidi asilimia 200 ikilinganishwa na mwaka 2019/20 (Tariff Application, Jedwali Na. 1, uk. 5–6).

Baraza linatambua kuwa, ongezeko la bei za pembejeo linaweza kuongeza gharama za kutoa huduma. Hata hivyo, ongezeko la bei za pembejeo pekee halitoshi kuthibitisha kiwango cha gharama kinachopaswa kurejeshwa kupitia bei. Ni muhimu kutofautisha kati ya ongezeko la bei ya pembejeo na gharama halisi inayotokana na kiasi cha pembejeo kinachotumika katika kutoa huduma.

Suala hili linahitaji kuangaliwa kwa makini zaidi kutokana na pendekezo la kuweka muundo mmoja wa bei katika eneo lote la huduma, wakati bei za sasa za Tanga City, Muheza na Pangani zinatofautiana. Nyaraka zilizowasilishwa hazijaonesha katika sehemu hii mgawanyo wa gharama za uendeshaji unaowezesha kutathmini gharama za kutoa huduma katika kila eneo. Kwa hiyo, Baraza linaona kuwa ni muhimu EWURA ijiridhishe kuwa gharama zinazokusudiwa kurejeshwa kupitia bei zimejengwa juu ya gharama halisi, zinazofaa na zenye ufanisi za kutoa huduma katika eneo lote la Tanga UWASA.

Aidha, tathmini hiyo inapaswa kuzingatia matumizi halisi kwa mujibu wa taarifa za fedha zilizokaguliwa, kiasi cha huduma kinachotarajiwa kutolewa, mwenendo wa matumizi katika miaka iliyopita na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka kuongeza ufanisi na kupunguza gharama zinazoweza kudhibitiwa.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kufanya tathmini ya kina ya makadirio ya gharama za uendeshaji na kujiridhisha kuwa kila gharama inayokusudiwa kurejeshwa kupitia bei ni ya lazima, ina ufanisi na inahusiana moja kwa moja na utoaji wa huduma;
 - ii. Kulinganisha makadirio hayo na matumizi halisi yaliyooneshwa katika taarifa za fedha zilizokaguliwa, mwenendo wa matumizi katika miaka iliyopita na kiasi cha huduma kinachotarajiwa kutolewa;
 - iii. Kujiridhisha kuwa Tanga UWASA imechukua hatua zinazofaa za kuongeza ufanisi na kudhibiti gharama zinazoweza kudhibitiwa kabla ya gharama hizo kuhamishiwa kwa watumiaji kupitia bei; na
 - iv. Kwa kuzingatia kuunganishwa kwa Tanga City, Muheza na Pangani chini ya muundo mmoja wa bei, kujiridhisha kuwa msingi wa gharama unaotumika kukokotoa bei unaakisi kwa usahihi gharama za kutoa huduma katika eneo lote na hautoi mzigo usio na uwiano kwa watumiaji wa eneo lolote.
6. Baraza limepitia viashiria vya utendaji vya Tanga UWASA na kubaini kuwa Mamlaka imeendelea kufanya vizuri katika baadhi ya maeneo ya kiutendaji. Kwa mujibu wa Mpango Biashara, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ulikuwa takribani asilimia 95 mwaka 2025/26, huku huduma ya maji ikitolewa kwa wastani wa saa 23.5 kwa siku kufikia Juni 2026 (Business Plan, uk. 34, 258–259 na Appendix C, uk. 372).

Hata hivyo, Baraza limebaini kutokuwiana kwa taarifa kuhusu ufanisi wa utoaji bili, ambapo sehemu moja ya Mpango Biashara inaonesha kiwango cha asilimia 87 kufikia Juni 2025, wakati sehemu nyingine inaonesha kiwango cha asilimia 81 kwa mwaka 2025/26. Aidha, Mpango wa Biashara umeweka lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji bili kutoka asilimia 81 hadi asilimia 95 ifikapo Juni 2031 (Business Plan, uk. 30; Appendix C, uk. 375; Implementation Plan, uk. 109).

Baraza limebaini pia kuwa kiwango cha maji yanayopotea/yasiyoingiza mapato kilikuwa takribani asilimia 28 mwaka 2025/26, na Mamlaka inalenga kukipunguza hadi asilimia 20 ifikapo mwaka 2030/31. Mpango Biashara huo pia unaeleza kuwa takribani kilomita 110 za mtandao wa maji katika Tanga City, Muheza na Pangani zimechakaa sana, hali inayochangia upotevu wa maji kutokana na uvujaji wa mara kwa mara (Business Plan, uk. 26–27; Financial Projections, uk. 243).

Katika kukabiliana na hali hiyo, Mpango wa Biashara umeweka hatua mbalimbali, ikiwemo kubadilisha kilomita 40 za mabomba yaliyochakaa, ambapo kilomita 25 zimepangwa Tanga City, kilomita 5 Muheza, kilomita 5 Pangani na kilomita 5 Mkinga. Aidha, Mamlaka inapanga kufunga vifaa vya kupima shinikizo la maji katika Tanga City, Muheza na Pangani na kufanya uchambuzi wa kitaalamu wa mtandao wa usambazaji katika maeneo hayo (Business Plan, Implementation Plan, uk. 106; Investment Plan, uk. 176).

Kwa upande wa madeni, wastani wa muda wa kukusanya madeni ya wateja ulikuwa miezi 3.6 mwaka 2025/26, wakati kiwango kinachopendekezwa ni kati ya mwezi mmoja na miwili. Mpango wa Biashara unaeleza kuwa hali hiyo inachangiwa na madeni ya taasisi za Serikali na wateja wa majumbani (Business Plan, uk. 257–259).

Kwa mtazamo wa Baraza, viashiria hivi vinaonesha kuwa bado kuna nafasi ya kuongeza ufanisi wa Mamlaka kupitia kupunguza maji yasiyoingiza mapato (yanayopotea), kuboresha utoaji wa bili na kuimarisha ukusanyaji wa madeni. Hatua hizi ni muhimu zaidi katika mazingira ambayo watumiaji wanaombwa kubeba ongezeko kubwa la bei.

Aidha, kwa kuwa sehemu ya miundombinu inayochangia upotevu wa maji ipo Muheza na Pangani, na Mamlaka yenyewe imepanga hatua mahsusi za kuboresha mtandao katika maeneo hayo, Baraza linaona kuwa ongezeko la bei linapaswa kuambatana na utekelezaji na ufuatiliaji wa maboresho hayo kwa kila eneo.

Baraza linaishauri EWURA mambo yafuatayo:

- i. Kujiridhisha kuhusu kiwango halisi cha ufanisi wa utoaji bili kitakachotumika katika tathmini ya mapato;
 - ii. Kuhusianisha utekelezaji wa bei mpya na malengo yanayopimika ya kupunguza maji yasiyoingiza mapato, kuongeza ufanisi wa utoaji bili na ukusanyaji wa mapato, na kupunguza muda wa kukusanya madeni;
 - iii. Kufuatilia utekelezaji wa hatua za kupunguza upotevu wa maji katika Tanga City, Muheza na Pangani, ikiwemo ukarabati na uingizwaji wa mabomba yaliyochakaa; na
 - iv. Kuhakikisha kuwa maboresho ya ufanisi yanayotarajiwa yanaonekana katika huduma zinazotolewa kwa watumiaji, hususan Muheza na Pangani ambako mabadiliko ya bei yanayoombwa yana athari kubwa zaidi.
7. Makadirio ya mapato na matumizi yaliyowasilishwa katika Ombi la Mapitio ya Bei pamoja na Mpango Biashara wa Tanga UWASA yanaonesha kuwa mafanikio ya bei inayopendekezwa yanategemea kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa makadirio ya uzalishaji na mauzo ya maji, ongezeko la idadi ya wateja na ukusanyaji wa mapato.

Mpango Biashara wa Tanga UWASA unaonesha pia kuwa, Mamlaka inalenga kuongeza uzalishaji wa maji kutoka wastani wa mita za ujazo 50,466 hadi 65,466 kwa siku, kuongeza idadi ya wateja kutoka 58,471 hadi 71,787, kuongeza kiwango cha huduma ya maji kutoka asilimia 95 hadi 99.5, pamoja na kupanua huduma za majitaka kutoka asilimia 3.4 hadi 30 katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango Biashara (Business Plan, Executive Summary, uk. vii–viii).

Aidha, Mpango Biashara huo umeweka malengo ya kuongeza wateja katika maeneo mbalimbali ya huduma, yakiwemo Muheza na Pangani. Miongoni mwa malengo hayo ni kuunganisha wateja wapya 150 kwa mwaka katika Mji wa Muheza na 100 kwa mwaka katika Mji wa Pangani (Business Plan, uk. 60; Implementation Plan, uk. 97).

Baraza linaona kuwa malengo hayo ni muhimu katika kupanua huduma. Hata hivyo, kufikiwa kwake kunategemea utekelezaji wa miradi kwa wakati, upatikanaji wa fedha, uwezo wa Mamlaka kuongeza uzalishaji na mauzo ya maji, pamoja na kufikiwa kwa idadi ya wateja wapya iliyokadiriwa.

Suala hili linahitaji kuangaliwa kwa makini zaidi kwa Muheza na Pangani, ambako, kama ilivyooneshwa katika Hoja Na. 2, tofauti kati ya wastani wa bei za sasa na wastani unaopendekezwa ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, ni muhimu kujiridhisha kuwa makadirio ya ongezeko la wateja, matumizi ya maji na mapato katika maeneo hayo yanaendelea kuwa halisi chini ya muundo mpya wa bei.

Baraza limebaini pia kuwa baadhi ya makadirio ya Mpango wa Biashara yamejengwa kwa dhana kwamba EWURA itaidhinisha bei kama ilivyoombwa na kwamba fedha kutoka Serikali na Washirika wa Maendeleo zitapatikana kwa wakati (Business Plan, Sehemu ya 1, uk. 2).

Hata hivyo, Baraza halikuona katika nyaraka zilizowasilishwa uchambuzi wa hali mbadala unaoonesha namna utekelezaji wa Mpango Biashara utakavyoathirika iwapo bei itaidhinishwa kwa kiwango tofauti na kilichoombwa, baadhi ya vyanzo vya fedha vitachelewa kupatikana, au malengo ya ongezeko la wateja, mauzo na ukusanyaji wa mapato hayatatafikiwa kama ilivyokadiriwa.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa makadirio ya uzalishaji, mauzo ya maji, ongezeko la wateja na ukusanyaji wa mapato yanaweza kufikiwa na yanaungwa mkono na mipango halisi ya utekelezaji;
- ii. Kujiridhisha mahsusi kuwa makadirio ya ongezeko la wateja na mapato katika Muheza na Pangani yanaendelea kuwa halisi kwa kuzingatia mabadiliko ya bei yanayopendekezwa katika maeneo hayo;
- iii. Kuitaka Tanga UWASA kuwasilisha uchambuzi wa hali mbadala unaoonesha athari endapo bei itaidhinishwa kwa kiwango tofauti, fedha za maendeleo zitachelewa, au uzalishaji, mauzo, wateja wapya na ukusanyaji wa mapato vitakuwa chini ya makadirio; na
- iv. Kuhakikisha kuwa mahitaji ya mapato yatakayorejeshwa kupitia bei yanajengwa juu ya dhana zinazoweza kuthibitishwa na kutekelezeka.

8. Baraza limepitia mapendekezo ya ada na gharama za kuunganishiwa huduma na kubaini kuwa Tanga UWASA inapendekeza ada ya kuunganishiwa huduma ya Shilingi 26,000 kwa makundi yote ya wateja (Tariff Application, Form 1B, uk. 10).

Hata hivyo, vielelezo vya bili za kuunganishiwa huduma vilivyowasilishwa vinaonesha kuwa kiasi cha mwisho anachoweza kulipa mteja hakihusishi ada hiyo pekee, bali kinaweza pia kujumuisha gharama za vifaa vinavyohitajika, uchimbaji wa mtaro, usafirishaji, kazi za kiufundi, ada ya usimamizi na Kodi ya Ongezeko la Thamani (Sample Connection Bills, uk. 5–8).

Kwa hiyo, kuwepo kwa ada ya Shilingi 26,000 pekee hakutoshi kuonesha gharama kamili ambayo mwananchi atalazimika kulipa ili kuunganishiwa huduma. Uwazi kuhusu gharama hiyo ni muhimu ili watumiaji waweze kufahamu mapema kiasi wanachotarajiwa kulipa na ili EWURA iweze kutathmini iwapo gharama hizo zinaweza kuwa kikwazo cha kupata huduma.

Suala hili ni muhimu pia kwa Muheza na Pangani, kwa kuwa Mpango wa Biashara umeweka malengo ya kuongeza wateja wapya katika maeneo hayo, yakiwemo maunganisho mapya 150 kwa mwaka Mji wa Muheza na 100 kwa mwaka Mji wa Pangani (Business Plan, uk. 60; Implementation Plan, uk. 97).

Kwa mtazamo wa Baraza, kufikiwa kwa malengo ya kuongeza wananchi wanaounganishiwa huduma hakutegemei upanuzi wa miundombinu pekee, bali pia gharama ambazo wananchi wanapaswa kulipa ili kuunganishiwa huduma. Hivyo, katika kutathmini gharama za kuunganishiwa huduma, ni muhimu kuangalia gharama kamili anayobeba mtumiaji, badala ya ada ya Shilingi 26,000 pekee.

Hivyo basi, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha iwapo Shilingi 26,000 ni ada ya msingi ya kuunganishiwa huduma pekee au inawakilisha sehemu gani ya gharama kamili anayopaswa kulipa mtumiaji;

- ii. Kuitaka Tanga UWASA kuweka wazi vipengele vyote vinavyoweza kujumuishwa katika gharama za kuunganishiwa huduma na msingi wa kukokotoa gharama hizo;
 - iii. Kujiridhisha kuwa gharama za vifaa, kazi, usafirishaji, uchimbaji na gharama nyingine zinazotazwa kwa mtumiaji ni halali, za lazima na zinaweza kuthibitishwa;
 - iv. Kutathmini iwapo gharama kamili za kuunganishiwa huduma zinaweza kuwa kikwazo kwa kaya zenye kipato cha chini kupata huduma; na
 - v. Kwa kuzingatia malengo ya kuongeza maunganisho mapya kwa Muheza na Pangani, kuhakikisha kuwa muundo wa gharama za kuunganishiwa huduma haukwamishi kufikiwa kwa malengo hayo.
9. Mpango wa Uwekezaji pamoja na vyanzo vya fedha vilivyoainishwa katika Mpango Biashara wa Tanga UWASA vinaonesha kuwa gharama ya utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano inakadiriwa kuwa takribani Shilingi bilioni 472.72, ikijumuisha gharama za uchakavu wa mali. Kati ya fedha hizo, takribani Shilingi bilioni 277.01 zinatarajiwa kutoka vyanzo vya ndani vya Mamlaka na Shilingi bilioni 195.71 kutoka vyanzo vya nje, ikiwemo Serikali na Washirika wa Maendeleo (Business Plan, Executive Summary, Jedwali Na. 1, uk. viii).

Aidha, Mpango Biashara unaonesha ruzuku za uwekezaji za takribani Shilingi bilioni 24.994 mwaka 2026/27 na Shilingi bilioni 153.880 mwaka 2027/28, pamoja na ruzuku nyingine katika miaka inayofuata (Business Plan, Executive Summary, Jedwali Na. 1, uk. viii).

Baraza linatambua na kuunga mkono mchango wa Serikali na Washirika wa Maendeleo katika kugharamia uwekezaji unaolenga kuboresha na kupanua huduma za maji na usafi wa mazingira. Hata hivyo, kwa kuwa sehemu ya mahitaji ya fedha ya Mpango Biashara inatarajiwa kugharamiwa kupitia mapato yatoakanayo na bei na sehemu nyingine kupitia vyanzo vya nje, ni muhimu kila mradi na chanzo chake cha fedha vitambuliwe kwa uwazi katika kukokotoa mahitaji ya mapato yanayotarajiwa kurejeshwa kupitia bei.

Uhakiki huo ni muhimu ili kuhakikisha kuwa gharama za uwekezaji zilizofadhiliwa kupitia ruzuku za Serikali au fedha za Washirika wa Maendeleo hazijumuishwi tena kama gharama zinazopaswa kurejeshwa na watumiaji kupitia bei. Aidha, uhakiki huo unapaswa kuhusishwa na uchambuzi wa Hati Fungani ya Kijani ulioelezwa katika Hoja Na. 4, ili kuwe na picha kamili ya chanzo cha fedha cha kila uwekezaji na gharama zinazopaswa kubebwa na watumiaji.

Kwa upande wa Muheza na Pangani, Baraza linaona umuhimu wa kuwa na uwazi kuhusu miradi inayotekelezwa katika maeneo hayo na chanzo cha fedha cha kila mradi. Mpango wa Biashara unahusu utoaji na uboreshaji wa huduma katika Tanga City, Muheza, Mkinga na Pangani. Kwa hiyo, pale uwekezaji katika Muheza au Pangani unapofadhiliwa kupitia Serikali, Washirika wa Maendeleo, Hati Fungani au mapato ya Mamlaka, chanzo hicho kinapaswa kutambulika wazi wakati wa kutathmini gharama zinazorejeshwa kupitia bei.

Kutokana na ukweili huo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa kila mradi wa uwekezaji umeainishwa pamoja na chanzo chake cha fedha, ikitenganisha fedha za ndani, ruzuku za Serikali, fedha za Washirika wa Maendeleo na vyanzo vingine vya ufadhili;
- ii. Kuhakikisha kuwa gharama za uwekezaji zilizofadhiliwa kupitia ruzuku za Serikali au fedha za Washirika wa Maendeleo hazijumuishwi tena katika mahitaji ya mapato yanayorejeshwa kupitia bei;
- iii. Kufanya mapitio ya uhusiano kati ya ruzuku za maendeleo, gharama za uwekezaji na mahitaji ya mapato yanayotarajiwa kurejeshwa kupitia bei, ili kuzuia watumiaji kubeba gharama zilezile zaidi ya mara moja;
- iv. Pale taarifa zinapopatikana, kuhakiki chanzo cha fedha na hatua ya utekelezaji wa miradi katika Tanga City, Muheza na Pangani, ili kuwe na uwazi kuhusu uwekezaji unaofadhiliwa kupitia bei na ule unaofadhiliwa kupitia vyanzo vingine; na

v. Kuhakikisha kuwa manufaa ya ruzuku na fedha nyingine za maendeleo yanaakisiwa ipasavyo katika uamuzi wa bei na katika maboresho ya huduma kwa watumiaji.

10. Baraza linatambua na kuunga mkono malengo ya Tanga UWASA ya kuboresha huduma katika kipindi cha Mpango Biashara. Miongoni mwa malengo hayo ni kuongeza kiwango cha huduma ya maji kutoka asilimia 95 hadi asilimia 99.5, kupunguza maji yasiyoingiza mapato hadi asilimia 20, kuongeza uzalishaji na idadi ya wateja, pamoja na kupanua huduma za majitaka kutoka asilimia 3.4 hadi asilimia 30 ifikapo 2030/31 (Business Plan, Executive Summary, uk. vii–ix).

Baraza linaona kuwa mafanikio ya bei mpya hayapaswi kupimwa kwa ongezeko la mapato ya Mamlaka pekee, bali pia kwa maboresho yanayoonekana na yanayopimika katika huduma wanazopata watumiaji. Maboresho hayo yanapaswa kujumuisha upatikanaji na mwendelezo wa maji, ubora wa maji, kupungua kwa maji yasiyoingiza mapato, kuongezeka kwa wananchi wanaounganishiwa huduma, kuboreka kwa huduma kwa wateja, pamoja na utekelezaji wa miradi ya majitaka na ulinzi wa mazingira.

Suala hili ni muhimu zaidi kwa Muheza na Pangani, kwa kuwa Mpango wa Biashara unaonesha uwekezaji na hatua mbalimbali zinazotarajiwa kutekelezwa katika maeneo hayo. Kwa mfano, katika upanuzi wa kilomita 60 za mtandao wa maji unaofadhiliwa kupitia Hati Fungani, kilomita 15 zimepangwa Muheza na kilomita 15 Pangani (Business Plan, uk. 369–370). Aidha, Mpango umeweka hatua za kubadilisha mabomba yaliyochakaa, zikiwemo kilomita 5 Muheza na kilomita 5 Pangani (Business Plan, Implementation Plan, uk. 106).

Mpango pia unalenga kuongeza wateja wapya 150 kwa mwaka Mji wa Muheza na 100 kwa mwaka Mji wa Pangani (Business Plan, uk. 60; Implementation Plan, uk. 97). Hivyo, kuna msingi wa kuweka viashiria vinavyoweza kupimwa kuhusu utekelezaji wa maboresho hayo katika kila eneo, badala ya kutathmini mafanikio kwa kutumia viashiria vya jumla vya Tanga UWASA pekee.

Kwa mtazamo wa Baraza, jambo hili lina umuhimu mkubwa kutokana na tofauti za athari za bei tulizobainisha katika Hoja Na. 2. Ikiwa watumiaji wa Muheza na Pangani watakabiliwa na mabadiliko makubwa zaidi kutoka viwango vya sasa vya bei, ni muhimu kuwe na uwazi kuhusu maboresho ya huduma yanayopangwa, muda wa utekelezaji na matokeo yanayotarajiwa katika maeneo hayo.

Baraza linaishauri EWURA yafuatayo:

- i. Kuhusianisha utekelezaji wa bei zitakazoidhinishwa na viashiria vinavyopimika vya ubora, upatikanaji, mwendelezo na ufanisi wa huduma;
 - ii. Kuweka, pale inapowezekana, malengo na taarifa za utendaji zinazotenganisha Tanga City, Muheza na Pangani, ili watumiaji waweze kuona maboresho yanayofanyika katika maeneo yao;
 - iii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi na maboresho yaliyopangwa mahsusi kwa Muheza na Pangani, ikiwemo upanuzi na ukarabati wa mtandao na ongezeko la wananchi wanaounganishiwa huduma;
 - iv. Kuitaka Tanga UWASA kuwasilisha taarifa za mara kwa mara kuhusu matumizi ya fedha, hatua za utekelezaji wa miradi na matokeo ya huduma; na
 - v. Kuhakikisha taarifa hizo zinapatikana kwa watumiaji ili waweze kuona kama ongezeko la bei linaambatana na maboresho ya huduma yaliyoahidiwa.
11. Mpango Biashara wa Tanga UWASA unaomnesha pamoja na kuboresha huduma za maji, Mamlaka imeweka mkazo katika kupanua huduma za usafi wa mazingira, kulinda vyanzo vya maji na kuimarisha miundombinu ya ukusanyaji na usafishaji wa majitaka. Miongoni mwa malengo yaliyowekwa ni kuongeza kiwango cha huduma za majitaka kutoka asilimia 3.4 hadi asilimia 30 ifikapo mwaka 2030/31 kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo (Business Plan, Executive Summary, uk. vii–viii; Section 5.5).

Baraza linaona kuwa maboresho hayo yana umuhimu mkubwa si tu katika kuongeza upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira, bali pia katika kulinda afya ya jamii, mazingira na vyanzo vya maji vinavyotegemewa na wananchi.

Hata hivyo, Baraza linaona kuwa mafanikio ya uwekezaji huo yatategemea utekelezaji wa miradi kwa wakati, upatikanaji wa fedha kama ulivyopangwa na ufuatiliaji wa karibu wa viwango vya huduma vilivyoahidiwa katika Mpango wa Biashara.

Kwa maoni ya Baraza, uamuzi wa kuidhinisha bei mpya unapaswa kwenda sambamba na mfumo madhubuti wa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya majitaka, utunzaji wa mazingira, ulinzi wa vyanzo vya maji na uzingatiaji wa viwango vya afya na mazingira. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa ongezeko la bei linaambatana na maboresho yanayoonekana na kupimika.

Baraza pia linaona kuwa taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Biashara na masharti ya Amri ya Bei zinapaswa kuwasilishwa kwa EWURA kwa wakati, zikitenganisha fedha zilizokusanywa, matumizi yaliyofanyika, hatua ya utekelezaji wa kila mradi na manufaa yaliyowafikia watumiaji.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira unaofadhiliwa kupitia bei, Serikali, Washirika wa Maendeleo na Hati Fungani ya Kijani unafuatiliwa kwa karibu ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata manufaa yaliyokusudiwa;
- ii. Kufuatilia kwa karibu upanuzi wa huduma za majitaka, uendeshaji wa mifumo ya ukusanyaji na usafishaji wa majitaka, ulinzi wa vyanzo vya maji na uzingatiaji wa viwango vya afya na mazingira;
- iii. Kuhakikisha kuwa Tanga UWASA inawasilisha kwa wakati taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Biashara na masharti ya Amri ya Bei (Tariff Order), zikiainisha matumizi ya fedha, hatua za miradi na matokeo kwa watumiaji; na
- iv. Kufanya tathmini ya mara kwa mara katika kipindi chote cha uhalali wa bei ili kuhakikisha kuwa manufaa yaliyotarajiwa yanawafikia watumiaji na kwamba

bei zilizoidhinishwa zinaendelea kuendana na kiwango cha huduma kinachotolewa.

12. Baada ya kupitia Ombi la Mapitio ya Bei la Tanga UWASA pamoja na Mpango Biashara na nyaraka zinazounga mkono maombi hayo, Baraza linaishauri EWURA kuzingatia yafuatayo kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu bei zinazoombwa:

- i. Kuitaka Tanga UWASA kuwasilisha uchambuzi wa athari za bei katika bili za watumiaji, ukitenganisha Tanga City, Muheza na Pangani, makundi mbalimbali ya watumiaji na viwango vya matumizi. Uchambuzi huo uzingatie pia athari za kuondolewa kwa madaraja ya matumizi na kuwekwa kwa muundo mmoja wa bei katika eneo lote la huduma. Hili ni muhimu kwa kuwa wastani wa bei za sasa unatofautiana kati ya Tanga City, Muheza na Pangani, wakati bei mpya inapendekezwa kwa eneo lote la huduma (Tariff Application, Form 1A, uk. 8–9).
- ii. Kujiridhisha kuhusu uwezo wa watumiaji kumudu bei zinazopendekezwa, kwa kuhusisha uchambuzi wa athari za bei katika bili na uwezo wa kaya kumudu gharama hizo. Tathmini hiyo izingatie mahsusi Muheza na Pangani kutokana na ukubwa wa mabadiliko kutoka wastani wa bei zao za sasa kwenda wastani unaopendekezwa, pamoja na kaya zenye kipato cha chini na watumiaji wenye matumizi madogo ya maji (Tariff Application, Form 1A, uk. 8–9; Business Plan, Executive Summary, uk. ix).
- iii. Kufanya uhakiki wa kina wa gharama zinazohusiana na Hati Fungani ya Kijani, ikiwemo riba, Mfuko wa Akiba wa Kulipa Hati Fungani, uchakavu wa mali na gharama za miradi, ili kuhakikisha kuwa gharama hizo zimeainishwa kwa usahihi na hazirejeshwi kwa watumiaji zaidi ya mara moja. Aidha, EWURA ihakiki hatua za utekelezaji, mgawanyo wa uwekezaji na manufaa ya miradi inayofadhiliwa kupitia Hati Fungani katika Tanga City, Muheza na Pangani (Tariff Application, uk. 4; Business Plan, uk. 369–370).

- iv. Kuruhusu kurejeshwa kupitia bei gharama za uendeshaji ambazo ni za lazima, zenye ufanisi, zimehakikiwa na zinahusiana moja kwa moja na utoaji wa huduma. Makadirio ya gharama yalinganishwe na matumizi halisi yaliyooneshwa katika taarifa za fedha zilizokaguliwa, mwenendo wa matumizi katika miaka iliyopita, kiasi cha huduma kinachotarajiwa kutolewa na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka kuongeza ufanisi (Tariff Application, Jedwali Na. 1, uk. 5–6).
- v. Kuhusianisha utekelezaji wa bei mpya na maboresho ya ufanisi wa Mamlaka, hususan kupunguza maji yasiyoingiza mapato hadi kiwango kilicholengwa, kuboresha utoaji na ukusanyaji wa bili na kupunguza muda wa kukusanya madeni. Aidha, utekelezaji wa hatua za kupunguza upotevu wa maji katika Muheza na Pangani, ikiwemo uingizwaji wa mabomba yaliyochakaa, ufuatiliwe kwa karibu (Business Plan, uk. 26–30 na 257–259; Implementation Plan, uk. 106 na 109).
- vi. Kuitaka Tanga UWASA kuwasilisha uchambuzi wa hali mbadala unaoonesha namna Mpango wa Biashara utakavyotekelezwa iwapo bei itaidhinishwa kwa kiwango tofauti na kilichoombwa, fedha za maendeleo zitachelewa kupatikana, au malengo ya uzalishaji, mauzo ya maji, ongezeko la wateja na ukusanyaji wa mapato hayatatafikiwa kama ilivyokadiriwa. Tathmini hiyo izingatie pia uhalisia wa malengo ya kuongeza wateja kwenye miji ya Muheza na Pangani (Business Plan, Sehemu ya 1, uk. 2; uk. 60; Implementation Plan, uk. 97).
- vii. Kuhakiki chanzo cha fedha cha kila mradi wa uwekezaji na kuhakikisha kuwa ruzuku za Serikali, fedha za Washirika wa Maendeleo na vyanzo vingine vya nje vinatambuliwa ipasavyo katika kukokotoa mahitaji ya mapato yanayorejeshwa kupitia bei. Hii ni muhimu ili kuhakikisha kuwa uwekezaji uliokwisha kugharamiwa kupitia vyanzo hivyo haujumuishwi tena katika gharama zinazobebwa na watumiaji. Mpango wa Biashara unakadiriwa kugharimu takribani Shilingi bilioni 472.72, ambapo takribani

Shilingi bilioni 195.71 zinatarajiwa kutoka vyanzo vya nje (Business Plan, Executive Summary, Jedwali Na. 1, uk. viii).

- viii. Kujiridhisha kuhusu gharama kamili za kuunganishiwa huduma, badala ya kuangalia ada ya Shilingi 26,000 pekee, na kuhakikisha kuwa vipengele vyote vya gharama vinawekwa wazi kwa watumiaji. Aidha, gharama hizo zisije kuwa kikwazo kwa wananchi kupata huduma, hususan katika Muheza na Pangani ambako Mamlaka imelenga kuongeza idadi ya wananchi wanaounganishiwa huduma (Tariff Application, Form 1B, uk. 10; Sample Connection Bills, uk. 5–8; Business Plan, uk. 60; Implementation Plan, uk. 97).
 - ix. Kuhusianisha bei zitakazoidhinishwa na viashiria vinavyopimika vya ubora na kiwango cha huduma, ikiwemo upatikanaji na mwendelezo wa maji, ubora wa maji, kupungua kwa maji yasiyoingiza mapato, ongezeko la wananchi wanaounganishiwa huduma, huduma kwa wateja na utekelezaji wa miradi ya majitaka na mazingira (Business Plan, Executive Summary, uk. vii–ix).
 - x. Kuitaka Tanga UWASA kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa miradi, matumizi ya fedha na matokeo ya huduma na, pale taarifa zinapopatikana, kuzitenganisha kwa Tanga City, Muheza na Pangani. Hii itaiwezesha EWURA na watumiaji kutathmini iwapo ongezeko la bei linaambatana na maboresho ya huduma katika maeneo wanayoishi.
13. Baraza linatambua umuhimu wa kuhakikisha Tanga UWASA ina uwezo wa kifedha wa kuendesha, kuboresha na kupanua huduma za maji na usafi wa mazingira. Hata hivyo, uendelevu huo unapaswa kwenda sambamba na ulinzi wa uwezo wa watumiaji kumudu huduma, ufanisi katika matumizi ya rasilimali na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma.

Kwa msingi huo, Baraza linaishauri EWURA kuhakikisha kuwa uamuzi wowote wa bei unazingatia tofauti za athari kwa watumiaji wa Tanga City, Muheza na Pangani, na kwamba ongezeko lolote litakaloidhinishwa linaambatana na maboresho yanayoonekana na yanayopimika katika upatikanaji, ubora, mwendelezo na uendelevu wa huduma.

Naomba kuwasilisha.